BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukuwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz


# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa kwa ajili ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026. Tunaomba Rehema za Mwenyezi Mungu ziendelee kutushukia ili tuweze kutimiza majukumu yetu ya msingi ya kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa kwa kipindi kilichobakia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo mkunjufu kabisa, nikushukuru wewe binafsi Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha hutuba hii ya maoni ya Kamati ya kudumu ya Ustawi wa Jamii kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026,

**Aidha,** Nichukuwe nafasi hii pia kuwapongeza wasaidizi wako Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa

pamoja mnavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa umahiri Mkubwa tokea kikao cha awali tulipoteuliwa mpaka sasa tunakwenda kuhitimisha kipindi chetu cha miaka mitano ya uongozi wetu, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kuhitimisha Baraza hili kwa Salama na Amani.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa uongozi wake wa busara uliojaa hekima. Tunamuomba Mola mtukufu amzidishie afya njema na maisha marefu na pia ampe ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu ili tuzidi kunufaika na uongozi wake kwa awamu inayofuatia.

**Aidha,** tunatoa pongezi za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla akiwa mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa pamoja wakimpatia Msaada mkubwa Mheshimiwa Raisi katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya uongozi wa nchi hii.

**Mheshimwa Spika,** Kwa Niaba ya wajumbe wenzangu wa kamati ya Ustawi wa Jamii napenda kutoa shukran za dhati kwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano tuliyokuwa nayo kwa kipindi chote cha miaka mitano tuliyokuwa pamoja katika kuhakikisha

tunamsaidia Mheshimiwa Rais katika Uongozi wake ulojaa mafanikio Zaidi ya asilimia mia ya malengo ya utekelezaji, Namuomba Allah atufanyie wepesi katika kinyanga'anyiro kwa awamu inayofuatia;
**Sambamba na hilo,** pia niwashukuru Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza Ndg. Raya Issa Mselem kwa mashirikiano makubwa waliokua wakitupatia Kamati kwa muda wote kwa lengo la kufanikisha shughuli za Baraza za kuisimamia Serikali katika utendaji kazi wa Mawizara.

**Mheshimiwa Spika,** Ni wajibu wetu kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Riziki Pembe Juma pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Anna Athanas Paul, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia kamati yetu wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara yao. Tunawaomba wazidishe mashirikiano ili kuimarisha utendaji wa shughuli zao za kila siku kwa lengo la kuleta ufanisi katika Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Pongezi za dhati nazitoa kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ambao wameweza kuijadili kwa kina na ipasavyo makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Heshima kubwa Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti. |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali (Jazeera) | Makamu Mwenyekiti. |
| 3. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe. |
| 4. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe. |
| 5. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe. |
| 6. | Mhe. Salma Mussa Bilali | Mjumbe. |
| 7. | Mhe. Chum Kombo Khamis | Mjumbe. |
| 8. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe. |
| 9. | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu Msaidizi. |
| 10. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu Msaidizi. |
| 11. | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo la Kikanuni, Kamati ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo sasa naomba nitekeleze jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa mwaka wa fedha **2025/2026** ina fungu **moja (1)** ambalo ni **H04** na imepanga kutekeleza **Programu Kuu Tatu (3) zenye Programu Ndogo Tano (5)** ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hizo ni **Shilingi Bilioni 17,072,042,000 (Bilioni Kumi na Saba, Milioni Sabiini na Mbili na Arubaini na Mbili Elfu)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Makadirio hayo ya matumizi tukilinganisha na mwaka wa fedha ulipita 2024/2025 yanaonekana kupungua kwa Wizara hiyo. Kamati imeelezwa kuwa kupungua huko kumetokana na kutopatikaNA kwa fedha za mradi wa maendeleo (PAMOJA).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kulikua na upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi kwa Wizara ya Maendeo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ilikadiriwa kutumia shilingi Bilioni **23,315,462,000/-** lakini hadi kufikia Machi 2025 Shilingi Bilioni **8,445,454,923/-** sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka zimepatikana, jambo ambalo limepelekea kutokukamilika kwa baadhi ya Huduma zilizopangwa katika baadhi ya Programu. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada walizochukuwa za kutoa huduma bora japo kuwa walikuwa na uchache wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kuwa Wizara inatekeleza kazi zake kwa utoaji wa huduma zaidi katika jamii, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukiboresha chanzo cha mapato ambacho ni Ukumbi wa Mikutano uliopo Sebleni utakaowezesha kuingiza mapato kwenye mfuko mkuu wa Serikalini, Hivyo Kamati imeitaka Wizara ya Ustawi wa Jamii kuimarisha zaidi ukumbi huo ili uwe na miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kuweza kufikia makusanyo ya mapato yaliyokadiriwa.

## PROGRAMU KUU HIFADHI YA JAMII (PH0401)

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia huduma mbili kuu; Kutoa huduma ya Ustawi wa Jamii na Uendeshaji wa Pencheni Jamii. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 3,643,223,000.00 sawa asilimia 21 ya bajeti ya Wizara. Kupitia Programu hii Wizara imepanga kutekeleza kazi mbali mbali zikiwemo; Kuendelea kutoa huduma za kiustawi kwa Wazee ikiwemo kufanyia kazi upatikanaji na matumizi ya vitambulisho na kuimarisha mabaraza ya wazee katika maeneo yao ya makaazi; Kuendelea na awamu ya pili ya matengenezo katika makaazi ya wazee Sebleni na kujenga upya makaazi ya wazee ya Welezo; na Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali juu ya jitihada za kuwaboreshea Wazee makaazi yaliyo Bora Limbani kwa Pemba na Sebleni kwa unguja. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia Ufadhili wa UAE wanatarajia kujenga makaazi kwa upande wa welezo Unguja. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara

kufuatailia kwa karibu Washirika hao wa maendeleo ili kuona ujenzi huo unaanza na kukamilika kwa wakati kwani Mradi huo ni wa muda mrefu umechelewa kuanza kutokana na changangamoto mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikikisha Wazee wanapata huduma bora na kwa haraka katika masuala ya kijamii, Wizara kupitia kifungu cha Huduma cha Ustawi wa Jamii (HH04010101) imetenga fungu kwa ajili ya kuendeleza zoezi la kuwatengenezea Vitambulisho Wazee wetu ili waweze kuvitumia na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wazee hao. Hivyo Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada hizo na inaishauri kuharakisha zoezi hilo likamilike kwa wakati ili vitambulisho hivyo viweze kutumika.

**Mheshimiwa Spika, Licha** ya kupungua kwa Bajeti kuu ya Wizara ambayo imepelekea kupungua kwa Fedha katika kifungu cha Huduma ya ustawi wa jamii (HH04010101), bado Kamati inaishauri tena Wizara kuangalia jinsi ya kuongeza kima cha fedha ili kuweza kuwasaidia wanafamilia wenye mazingira magumu zaidi kwani kiwango cha fedha cha Tzsh. Elfu 30,000/- kinachotolewa kwa familia nzima kwa kila mwezi ni fedha ndogo mno na haikidhi haja katika kuwapunguzia ugumu wa maisha katika familia hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika kifungu cha huduma cha uendeshaji wa pencheni jamii HH04010102 ambapo makadirio ya fedha hizo hayakuweza kupatikana, makadirio ya kifungu hicho katika mwaka wa fedha 2025/2026 yamepungua zaidi kutoka Tzsh. 30,360,000 hadi kufikia Tzsh. 27,040,000/-. Kamati inaishauri Wizara ya Ustawi wa Jamii kukaa pamoja na kitengo cha Bajeti na Mipango cha

Wizara husika ili kuhakikisha Fedha itakayopangiwa kifungu hichi inakidhi malengo katika ufuatiliaji wa wazee ili kufikia lengo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kila Mzee anayestahili kupata Pencheni awe anapata tena kwa wakati.

### PROGRAM KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI (PH0402)

**Mheshimiwa Spika,** Program hii ina jumla ya program ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba. Katika utekelezaji wa Bajeti ya wizara imepangiwa Bil. 7,691,816,000/= sawa na asilimia 45 kutumiwa kwenye fungu kuu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji kifungu (SH040201) kimeongezeka kwa ujumla wake kutoka Bil 4,738,047,000/- kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia Bil 5,553,920,000/- kwa mwaka wa fedha 2025/2026 hii inatokana kifungu cha Huduma za Utawala na Uendeshaji (HH04020203) kuhamishiwa katika kifungu (HH04020102) .

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuwaendeleza watendaji wake kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi hasa kwenye masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na masuala yanayohusiana na jamii ili waje wawe msaada kwenye kutoa elimu na kutatua changamoto zinazokabiliana na jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia kuchelewa kuanza kwa Mradi wa Pamoja, Kamati imeelezwa kwamba kulikua na baadhi ya vipengele vilikua havijakaa sawa pia na Serikali kutaka kujiridhisha kwanza kama Mradi huu utakua na Tija kwani ni mradi utakaotumia Fedha nyingi tena za Mkopo ambapo kwa sasa tayari uchunguzi na hatua zote zimekamilika na umeshapatiwa baraka zote kutoka Serikalini na unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Hivyo Kamati inawashauri watendaji wa Wizara kuwa na mashirikiano ya Pamoja katika utekelezaji wa Mradi huu sambamba na kuzitumia Fedha za Mradi kwa malengo yalivyowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara kifungu **SH040202** kimepungua kwa ujumla wake kwa mwaka wa fedha 2025/2026, hali hii imesababishwa kutokana na fedha za Mradi wa Pamoja kuhamishimiwa moja kwa moja katika huduma husika zinazoenda kutekelezwa, kama vile kwenye huduma ya Maendeleo ya Jinsia na Uwezeshaji Wanawake (HH04030201) ambapo kwa mwaka wa fedha uliopita 2024/2025 makadirio ya fedha zote za Mradi huu ziliingizwa katika Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara zimepangwa Tzsh. 5,737,003,000 sawa na asilimia 34 kutumika katika fungu la Programu Kuu hii.  Miongoni mwa majukumu ya program hii ni Kuyafikia Majukwaa yote ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kuanzia ngazi ya Shehia hadi Mikoa; Kuendelea kuwajengea uwezo wanawake kuweza kuchukua

fursa mbali mbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii; Kuhamasisha Wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali; Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kumaliza na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto na Kuadhimisha siku za kimataifa na kikanda.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza wizara kwa kuongezeka kwa Makadirio ya Fungu PH0103 katika Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia kutoka Tzsh 2,392,112,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia Tsh 5,737,003,000 katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Fedha hizo zinatarajia kutekeleza shughuli mbali mbali kama kuwezesha wanawake kiuchumi, kupinga na kukabiliana na vitendo vya kikatili na udhalilishaji wa kijinsia nakadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutoa Elimu zaidi juu ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji na jamii kuondoa muhali katika kusaidia kutoa ushahidi ili kuepuka madai ya kesi za udhalilishaji kumalizwa kienyeji na kutofikishwa kwenye vyombo vya sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, napenda kuchukua fursa hii ya kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba Kamati ya Ustawi wa Jamii naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

……………………………,

**Sabiha Filfil Thani,**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**